

Moyo Wa Mtoto



Tumaini la Maisha

*Thank you also to our patron Fr Terry Cantwell for the
beautiful translation from English to Swahili.*

Hospitali ya Taifa Muhimbili

Moyo Wa Mtoto



Imeongozwa na Dr. Trish Scanlan (Paediatric Oncologist)

Wapiga Picha Gaudence Kikwembe & LeslieKH Photography

Imeandikwa na Angelica Spence

Kwa ajili ya watoto wa wodi ya Upendo



Kitabu hiki ni kwa ajili ya watoto wa wodi
ya Upendo katika Hospitali ya Taifa
Muhimbili. Ni habari ya Moyo wa mtoto na
safari yake tangu kupimwa kuwa na
cancer hadi kutibiwa hata kupona kabisa.








Habari! Jina langu ni moyo wa mtoto.



Mimi ni “Kijidubu” naishi kijijini pamoja
na baba na mama.



Nasaidia kazi za kuchunga ng’ombe,
 na kila siku naenda shulen!





Napenda kwenda shulen.



Shulen hua nacheza pamoja na marafiki zangu.

Pia nasoma na kuchora picha kwa kutumia
penseli za rangi.



Lakini leo sijisikii vizuri.



namwambia mwalimu kwamba nataka kurudi

nyumbani.



Mama ananipeleka
hospitalini ili nikapimwe
na daktari.



Nakaa katika chumba cha
kusubiri hadi daktari
anakuwa tayari kunipima.



Nesi mzuri akaja anongea na
mama wakati ananipima joto.





Halafu akaja daktari naye
vilevile ni mwema
ananiuliza maswali mengi.

Daktari anachunguza kinywani (mdomoni) mwangu, anasikiliza moyo unavyopiga na anapapasapapasa tumbo langu.

Ninaogopa kidogo lakini wote katika hospitali wanakuwa wema sana na mama anakua pamoja nami muda wote.



Nadhani huyu daktari anajua hali yangu mbaya.
Ananivisha kidoleni kijidudu fulani – hakiumi lakini
kinatoa sauti “beep beep”. Daktari ananiambia
“utajisikia nafuu ukivishwa karokoa (mask)
ipulizayo hewa baridi”.



Mimi sitaki hiyo karokoa
(mask), namwambia
mama aitoe. Lakini
cha ajabu baada ya
muda mfupi naanza
kujisikia nafuu. Huenda
hii karokoa (mask)
inasaidia!





Baadae nesi alinipatia kitanda
kikubwa katika chumba kiitwacho
'wodi'. Humu nawaona watoto
wengine na baba na mama zao.
Mama analala pamoja nami na
ananikumbatia. Hapo daktari
akamwambia mama ni lazima apate
vipimo. Kipimo cha kwanza
anachotaka ni cha damu yangu.

HATARI!! 😞



OUCH! Inauma kwa
dakika moja tu na
nikalia kidogo.



Mama na daktari wote
wakaniambia kuwa
nimekuwa hodari. Kisha
nakafungiwa plasta kidoleni.




Baada ya hapo nikaenda mahala pengine na
huko kuna machine makubwa makubwa –
yana mjina mrefu ambayo sasa siyakumbuki.



Yanatisha lakini kumbe ni kamera kubwa tu!
Yanapiga picha ya vitu vya ndani ya mwili.






Katika kipimo kimoja wakanipaka jeli baridi tumboni. Kwakuwa nilikuwa nasikia joto sana, nilivyo pakwa hiyo jeli nilijisikia vizuri sana – iliuwa kama wamenipaka barafu.




Kipimo kifuatacho kinaitwa
X-ray, nikalala chali na
kutulia na kuangalia taa
ndogo. Muda si muda
kipimo kimemalizika.



Wow - Haikuuma hata
kidogo!





X-ray yangu
inaonekana hivi!



Pia wakaniweka katika machine ya ajabu
yenye kelele nyingi yenye mfano wa pipa
kubwa.



Nikaogopa tena lakini muda wote mama
anakuwa pamoja nami, na kinachotokea ni
meza niliyolalia kuchezacheza na mashine
kutoa sauti! Haiumi hati kidogo – hadi nasinzia
kwa muda mfupi.



Ili madaktari waweze kuniponya nikafanyiwa
vipimo vingine – kimoja ni kipigwa sindano ya uti
wa mgongo na cha pili ni cha uboho wa mfupa.

Lakini ajabu sikumbuki hata kidogo. Daktari
alinipa dawa ya usingizi na nilipoamka, vipimo
vyote vimekwishapita. Ilibaki plasta tu mgongoni.

Nesi amempa mama chombo kütwacho ‘pima joto’ akasisitiza umuhimu wa mama kupima joto ya mwili wangu.



Joto likipanda juu hadi 38, lazima amwite nesi naye atamwita daktari. Inaonekana kama ni muhimu sana.

Siku chache baada ya kumaliza vipimo
madaktari walikaa na mama na
wakamwambia kuwa ninaumwa na ugonjwa
uitwao '**cancer**'. Wakamwambia watanitibu
hana na nitapata kupona kabisa.



Daktari anamwambia mama lazima nitibiwe na dawa inayoitwa ‘chemotherapy’. Dawa hiyo inatolewa kwa vidonge au kwa dripu.



Baada ya kutibiwa kwa hiyo dawa wakati mwingine najisikia vizuri, wakati mwingine najisikia vibaya. Wakati mwingine nataka kucheza, wakati mwingine nataka kulala tu. Mama ananitunza muda wote.

Siku moja nilistuka kuona nimepata kuwa kipara, nywele zangu zote zimetoka! Mama aliniambia kwamba ni matokeo ya kula dawa hiyo – dawa hiyo inapigana na seli mbaya mwilini mwangu.



Karibu nitajisikia nafuu na nitataka kucheza tena.



Ninafurahia kuchora
kwa rangi pamoja
na rafiki zangu



Wapo watoto wengine
wengi kwenvye wodi na
ninafurahi kupata marafiki



Siku moja nikajisikia nimechoka sana. Nesi akaleta mfuko wa damu na nikaangalia wakati damu inatiwa katika mkono wangu – WOW! Mara ilipokwishatiwa nilijiona kujaa nguvu – ni kama ninaamka baada ya kulala usingizi mnono.





Baada ya wiki chache daktari akamwambia mama kwamba ni lazima nitiwe operesheni ili kuondoa uvimbe uliosababisha niumwe. Inatisha! Mama akakaa pamoja nami na kueleza ugonjwa nilionao na kwamba nikitiwa operesheni hiyo nitapata nafuu zaidi.



Mama na nesi walinivesha shati la kijani na sote pamoja tukaanza safari ya kwenda ng'ambo ya hospitali. Nesi akanisafirisha hali ninalala juu ya kitanda chenye magurudumu – wee – hata tukafika chumba cha operesheni kiitwacho “theatre”.

Baada ya kutiwa operation,

nikarudia
tena kitanda
change
katika wodi
ya Upendo.



Nimefungiwa
bandeji tumboni
na napewa
dawa ili nijisikie
nafuu zaidi.
Manesi
wananitunza kila
saa.

Nilichopenda hasa katika matibabu yangu, ni
uji mtamu niliopewa kujenga mwili



niwe na nguvu na ushujaa katika kushinda
cancer.

Baada ya kufanyiwa operesheni nikapewa “chemo” neno tunalotumia kwa dawa katika wodi ya Upendo. Lakini kila siku naenda shulen. Nawapenda walimu na wachekeshaji ni wazuri.



Nasi tunapewa nafasi ya kucheza nje wakati wakubwa wanasoma.





Usiku mmoja saa za katikati nilijisikia mwili una joto sana na mara tena kuwa na baridi sana. Nikaanza kutetemeka. Mama akatumia pima joto na kuona 38. Mama akatambua kuwa ni juu mno na ni hatari. Akamwita nesi ingawa ni usiku wa manane. Daktari akaja haraka. Nahitaji kupimwa damu na dawa iongezwe katika dripu kila mda.

Vilevile nikapewa

oksijeni

kwasababu

inanisaidia

kupona.



Inachukua mda kidogo hadi najisikia nafuu.

Ninafurahi na kuona nina bahati. Mama
alitumia akili kufanya haraka kuwaita nesi na
daktari.



Kijiji chetu mbali na hospitali. Kwa hiyo wakati najisikia nafuu na ninapumzika kula dawa, twaweza kukaa katika Ujasiri house. Ujasiri house ni kama nyumbani ingawa tuko mbali na kijiji chetu.






Hapa nimepata
marafiki wengi




Hiki ni kitanda chetu,
cha mimi na mama
katika Ujasiri House





© LeslieKH Photography

© LeslieKH Photography



Ninapokaa katika Ujasiri house ninapata nafasi ya kucheza ndani na nje. Tena kuna nafasi ya kujifunza kushona na vilevile kuchora kwa penseli za rangi pamoja na rafiki zangu.



Mimi na mama tunakwea
basi na kwenda hospitali ya
“Ocean Road Cancer
Institute” (ORCI) kupata tiba
ya ‘Radiotherapy’.

Sasa tumerudi wodini na nikupewa vipimo
na matibabu ya mwisho kabla ya kwenda
nyumbani.



Nikakutana na
daktari kwa mara
ya mwisho.



Daktari ameridhika
sana na hali yangu,
naye mama
anafurahi. Imekuja
saa ya kurudi
nyumbani.



Nafurahi mno kuwa tunakwenda nyumbani.
Ingawa ni lazima niwaache marafiki wengi
hapa. Mama akaahidi kuwa tatarudi mara kwa
mara. Haya kwaherini na asanteni wote!! 😊



